# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA WAZIRI MKUU

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## JANGWANI SEKONDARI

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU– TAMISEMI**

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule 0762828626**

**Makamu Mkuu wa Shule 0758655393/0652659696**

**Matron-0687128092**

**Shule ya Sekondari Jangwani,**
**S.L.P 2276,**
**DAR ES SALAAM.**

**Tarehe ....................……………**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI JANGWANI HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM, MKOA DAR ES SALAAM MWAKA .....................**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka .......... na atasoma tahasusi ya PCB, CBN, HGE na EGM.

Shule ya Sekondari Jangwani ipo umbali wa Kilometa tatu (3) kutoka katikati ya Jiji, usafiri wa basi unapatikana kwa urahisi katika kituo cha mabasi cha Magufuli, kisha tumia usafiri wa mwendokasi (DART) hadi kituo cha Fire, nauli kwa mwanafunzi ni shilingi 200 (mia mbili tu).
Muhula wa Masomo unaanza tarehe ........................
.......hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ......................
Mwisho wa kuripoti ni tarehe …………….

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni :-

(a) **Wanafunzi wasiovaa hijabu**

- Sketi mbili za rangi ya karoti **iwe nchi tano chini ya goti**.
- Mashati mawili meupe ya **mikono mifupi**.

(b) **Wanafunzi wanaovaa hijabu**

- Sketi mbili ndefu za rangi ya karoti zinazofunika vifundo vya miguu
- Mashati mawili ya mikono mirefu, yanayofunika makalio (**isiwe nusu kanzu**)

**ANGALIZO**:-

- Sare hizi zisiwe za kubana mwili.
- Juba lifunike vifundo vya mikono na livuke nyonga/ kitambaa cha halua **cheupe** kitumike.

(c) **Sare za michezo**

**Sare za michezo**

- **T**-Shirt ya rangi ya blue (form Six) yenye nembo.
- Bukta sketi ya rangi ya karoti.

(d) Sweta la rangi ya njano yenye ufito wa karoti kwenye shingo na mikononi. (**baby yellow**)

(e) Viatu

Raba nyeupe zenye gidamu (kamba) zisizo na maandishi wala alama yeyote, pia zisiwe na soli nene.

(f) Soksi

Nyeupe zisizo na alama wala maandishi, zisivuke goti.

**Michoro ya sare hizi ipo katika kielelezo namba 1**.

(g) Mwanafunzi awe na nywele fupi zinazochanika kwa kitana kidogo.

**Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 10 (*Quire 3*);
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (tazama kielelezo namba 2.)
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator **yenye Function 991**.
vi. Ndoo 1 ndogo (lita Kumi) yenye mfuniko;
vii. Jembe,Squeezer na ARO.

**2.2 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**b) Shule za Kutwa**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 35,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **50,000/=** |

**Malipo yafanyike kwenye akaunti ya shule CRDB No 0150251317600. Jina Jangwani sekondari.**

**c) Chakula kwa wanafunzi wa Kutwa**

Mwanafunzi atatoa shilingi 20,000 kwa mwezi kwa ajili ya chakula cha mchana (kwa mujibu wa mwongozo wa Wizara ya Elimu.) Fedha itakabidhiwa shuleni siku atakayoripoti.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

- ❖ Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

- ❖ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
vii. Uvutaji wa sigara;

viii. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
ix. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
x. Kusababisha mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu, pamoja na picha tatu za mwanafunzi za karibuni (passport size) apige akiwa amevaa shati la shule.

**5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII!**

**Saini ya Mkuu wa Shule** ..............................

**Jina la Mkuu wa Shule NYAIBULI BHOKE NYAGONDE.**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule**

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI

UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- **Mkuu wa shule :0762828626**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0758655393/0652659696**
- **Mwandamizi Taaluma: 0719570802**
- **Mwandamizi Malezi :0717175688**

## FOMU RASMI YA KUANDIKISHWA

PICHA YA MWANAFUNZI

**Sehemu hii ijazwe na mwanafunzi: -**

1. Majina kamili ya mwanafunzi: [Matatu] ………………………………………………
2.Uraia: -………………………………………………………………………………….
3.Dini: - ……………………………………………………………………………...
4. Tarehe ya kuzaliwa na Namba ya cheti cha kuzaliwa:- ………………………………
5. Mkoa/Wilaya asili ya mwanafunzi: - ………………………………………………….
6. Sio yatima/Yatima/ Mzazi mmoja, Kama mzazi mmoja ni baba tu/ mama tu [**Kata isiyohusika**]
7. Shule uliyosoma kabla ya kuja Sekondari ya Jangwani

| **MAJINA MATATU YALIYOANDIKISHWA SHULENI** | **SHULE YA SEKONDARI ULIKOSOMA** | **MWAKA ULIOANZIA** | **MWAKA ULIOTOKA** |
|---|---|---|---|
| | | | |

KAMA MUHAMIAJI TAARIFA ZA UHAMIAJI

| SHULE ULIYOTOKA | WILAYA | MKOA | KIDATO | TAREHE |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

Prem No. yako ni ……………………………………….

Mawasiliano ya Mkuu wa Shule ulikotoka ………………………………….............

Sahihi ya mwanafunzi …………………………. Tarehe ……………………………

PICHA YA MZAZI/MLEZI

**Sehemu hii ijazwe na Mzazi/ Mlezi:-**

1. Jina kamili la mzazi/ mlezi:- ………………………………………………………………
2. Uraia ………………………. Namba ya cheti cha uraia ……………………………….
3. Anuani kamili ya makazi [ Mtaa, Kata, Wilaya ] ……………………………………….
   ……………………………………………………………………………………………..
4. Namba ya simu ya baba/ mlezi …………………………………………………………
5. Namba ya simu ya mama/ mlezi ……………………………………………………..
6. Kazi anayofanya mzazi/ mlezi ( kama vile Daktari, mwalimu, fundi n.k) ………………….....................

PICHA YA NDUGU MWINGINE

**Ndugu wengine wa karibu :-**

| | Jina la ndugu | Anapoishi | Uhusiano | Namba ya simu |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |

Sahihi ya mzazi/ mlezi ……………………………... Tarehe …………………………...

## AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi ………………………………………………………………………… ( Majina matatu )

1. Nimeyasoma na kuyaelewa maelezo yote na nimekubali kujiunga na shule ya Sekondari ya Jangwani kuanzia tarehe ………………………………….

2. Naahidi kwamba :-

a) Niitazingatia sheria zote za shule na kutimiza wajibu wangu kama mwanafunzi.

b) Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo vilivyo kinyume na sheria za shule na sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

c) Nitatunza mali ya Umma ambayo ni pamoja na Majengo, Samani, Vitabu , vifaa vya maabara na vifaa vinginevyo nitakavyokabidhiwa.

d) Nipo tayari kuchukuliwa hatua yeyote stahiki endapo nitakiuka maelekezo yaliyotolewa kwenye fomu hii.

Saini ya mwanafunzi: ………………………………. Tarehe: ……………………………

## AHADI YA MZAZI/ MLEZI

Mimi …………………………………………… Ni Mzazi/ Mlezi wa ……………………………………

wa kidato cha ………… mwaka ………………... naahidi kwamba: -

1.Nitashirikiana kikamilifu na uongozi wa shule na walimu wote kwa ujumla katika kumuelimisha na kumlea mtoto wangu. Hii ni kuhakikisha kuwa atazitii sheria zote za shule na kuyazingatia mambo yote yaliyotajwa.

2. Nitafanya kila niwezalo kumwezesha mwanangu kufika shuleni kila siku saa kabla ya saa 1:00 asubuhi.

3. Nitajitahidi kadiri ya uwezo wangu kuhakikisha mwanafunzi anahitimu kidato cha nne/ sita. Yaani anasoma hadi anamaliza kadiri inavyotakiwa.

4.Ninaruhusu mwanangu achukuliwe hatua yeyote stahiki endapo atavunja mojawapo ya sheria na kanuni zilizoorodheshwa.

Saini ya Mzazi/ Mlezi ………………………………… Tarehe …………………………

**PRIME MINISTER'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**ILALA MUNICIPAL COUNCIL**

Head of School's Office,
P. O. BOX 2276,
DAR ES SALAAM.

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

PART A.

To the medical officer ________________________________

Miss ________________________________________

Please examine the above named student for her full time secondary school studies.

Date ___________________________ Signature _________________________

**Headmistress.**

PART B.

MEDICAL CERTIFICATE

(**To be completed by a medical Officer at a Healthy Centre level and above**)

Put a tick (√) for positive and a cross (×) for negative in a box provided.

| | |
|---|---|
| Pregnancy | |
| Asthma | |
| Sight | |
| Diabetes | |
| Worms (Stool Test) | |
| Epilepsy | |
| T.B (Tuberculosis) | |
| Sickle Cell | |
| Heart Disease | |
| Yellow Fever | |
| U.T.I | |
| Venereal Diseases | |

| | |
|---|---|
| Leprosy | |
| Other Problems and Physical Impairment | |

**I have examined the above named student and concluded that she is physically fit for full time secondary school studies.**

Date ____________________ Signature ______________________

Station ______________________ Designation _____________________ Official Stamp

**KIELELEZO NAMBA 2**

